HABARI LEO UK 15.

# Mapato ya uvuvi Mkinga yafikia mil. 97/-


Na Mwandishi Maalumu, Tanga

MAPATO ya Halmashauri ya Mkinga mkoani Tanga kupitia sekta ya uvuvi yamepanda kufikia Sh milioni 96.6 mwaka 2019/ 2020

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga, Rashid Gembe amesema mapato hayo yamepanda kutokana na mikakati waliyoiweka dhidi ya uvuvi haramu.

Alibainisha hayo wakati akizungumza na timu ya wataalamu kutoka Mradi wa Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIO-fish) ofisini kwake mwishoni mwa wiki. Alisema mwaka 2015/ 2016 kabla ya mradi huo kuanza kuhamasisha uvuvi endelevu na wenye tija, Halmashauri ya Mkinga ilikusanya Sh milioni 45.3 kutoka katika sekta ya uvuvi.

Gembe aliwaeleza wataalamu hao wanaofuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo wilayani humo kuwa mradi



huo umekomesha uvuvi haramu hususani uvuvi wa kutumia mabomu na makokoro.

"Mradi wa SWIOfish ulipoanza kufanya kazi wilayani kwetu mwaka 2016 ulianzisha Vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari (BMU) vipatavo 14 ambavyo vimekuwa vikitoa elimu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa wananchi ikiwemo kutunza mazingira ya fukwe za bahari," alisema na kuongeza:

"Pia mradi ulimarisha doria za baharini na nchi kavu kwa lengo la kulinda rasilimali za uvuvi, doria hizo zimepunguza uvuvi haramu na sasa mapato ya halmashauri yameanza kupanda kwa sababu wavuvi sasa wanafanya uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi".

HABARI LEO UK 20.

# *Tanzania yazalisha chanjo sita za mifugo *

Na Mwandishi Wetu, Kibaha

TANZANIA imepiga hatua kubwa katika uzalishaji wa chanjo za mifugo, baada ya kuzalisha chanjo sita katika muda mfupi.

Aidha, chanjo ya saba inatarajiwa kufanyiwa majaribio ya mwisho hivi karibuni baada ya kuanza majaribio ya awali.

Hayo yalisemwa mjini hapa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, alipofanya ziara katika taasisi mbili zinazohusika na chanjo za mifugo akiwa na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Taasisi alizotembelea ni Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) na Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI).

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk Furaha Mramba, tangu uzalishaji wa chanjo hizo uanze rasmi mwaka 2014, wameshatengeneza chanjo sita. Alisema TVI ilianza kwa kuzalisha chanjo moja ya ugonjwa wa mdondo wa kuku yenye jina la kibiashara la Temevac.

Alisema hadi kufikia mwaka huu wamezalisha chanjo aina sita ambazo ni dhidi ya ugonjwa wa mdondo kwa kuku na ya dhidi ya ugonjwa wa kimeta kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Nyingine ni chanjo dhidi ya ugonjwa wa chambavu kwa ngombe, mbuzi na kondoo na chanjo dhidi ya ugonjwa wa kutupa mimba kwa ngombe, chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe.

Chanjo ya sita aliitaja kuwa ni ya dhidi ya mchanganyiko wa kimeta na chambavu kwa ajili ya kukinga mifugo na magonjwa hayo mawili kwa pamoja.

"Lengo la wakala ni kupanua wigo wa aina za chanjo zinazozalishwa kwa kulingana na mahitaji, ingawa unaweza kuongeza hadi kufikia milioni 100," alisema.

Dk Bitanyi alisema endapo watapatiwa vifaa zaidi wataweza kuzalisha chanjo nyingi zaidi na hata kuuza nje ya nchi kwani zina ubora wa hali ya juu.

Alisema katika maeneo ya mipakani imegundulika chanjo ya mdondo inavushwa nchi za jirani za Malawi, Burundi na Kenya kwa njia ya magendo kutokana na ubora wake.

Kwa upande wake, Profesa Ole Gabriel alisema uzalishaji wa chanjo hapo nchini una faida kubwa.

Alizitaja kuwa ni usalama wa nchi hasa kutokana na kuwapo kwa uhusiano mkubwa kati ya afya ya binadamu na ya mifugo.

Aliwataka wafugaji kutumia chanjo zinazozalishwa na TVI kwani zina ubora na zinapatikana kwa gharama nafuu.



---

**JAMHURI YA MUUNGANO**
**WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya **UCHIRA**
usimamizi wa mirathi **Na.9/2020**
Ombi la **IVYOLATA JAMES KUWDY** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu:
**JAMES FABIAN KUWDY KIRUA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka, mnamo tarehe **15/10/2020** kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

14/9/2020

1303280001

---

**JAMHURI YA MUUNGANO**
**WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya **ARUSHA MJINI**
usimamizi wa mirathi **Na.278/2020**
Ombi la
1. **EZEKIEL MICHAEL KIOLOGWE**
2. **VIVIENNE JR KIOLOGWE**

Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu:
**JAMESON REXFORD KIOLOGWE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI YA HII TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka, mnamo tarehe **28/10/2020** kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

1316220009

Scanned with CamScanner

kufichua vitendo hivyo.


Rose alisema mradi huo, utajikita

ambalo lisipodhibitiwa mapema

sauti zao, ikiwa ni pamoja na

na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).

MAJIRA UK 10.



**Mgeni rasmi katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Unywaji wa Maziwa Shuleni, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (aliyevaa miwani kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa shule za msingi walioshiriki maadhimisho hayo yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. Katikati ni Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel (kushoto kwake) Kaimu Msajili, Bodi ya Maziwa Tanzania, Noel Byamungu.** (Na Mpigapicha Wetu)

# Kupungua uvuvi haramu kwapaisha mapato Mkinga

**Na Mbaraka Kambona, Tanga**

MAPATO ya Halmashauri ya Mkinga, Mkoani Tanga kupitia Sekta ya Uvuvi yamepanda kufikia shilingi Milioni 96.6 mwaka 2019/2020 kufuatia mikakati waliyoiweka dhidi ya Uvuvi haramu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga, Rashid Gembe wakati akiongea na timu ya Wataalamu kutoka Mradi wa Ulinzi Shirikishi wa rasilimali za bahari kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (SWIOfish) ofisini kwake mwishoni mwa wiki alisema kuwa kabla ya mradi huo kuanza kuhamasisha uvuvi endelevu na wenye tija, mwaka 2015/ 2016 Halmashauri ya Mkinga ilikusanya kiasi cha shilingi Milioni 45.3 kutoka katika sekta ya Uvuvi.

Gembe aliwaeleza wataalamu hao waliokwenda kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo Wilayani humo kuwa mradi umechangia kwa kiasi kikubwa kukomeshwa kwa uvuvi haramu hususani uvuvi wa kutumia mabomu na makokoro.

"Mradi wa SWIOfish ulipoanza kufanya kazi hapa Wilayani kwetu mwaka 2016 ulianzisha Vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari (BMU) zipatazo 14 ambazo zimesaidia kutoa elimu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa wananchi ikiwemo kutunza mazingira ya fukwe za bahari," alisema Gembe.

"Pamoja na kuimarisha BMU hizo, pia iliimarisha Doria za Baharini na nchi kavu kwa lengo la kulinda rasilimali za uvuvi, na nikiri kuwa Doria hizo zimesaidia kupungua kwa uvuvi haramu na sasa mapato ya Halmashauri yameanza kupanda kwa sababu wavuvi sasa wanafanya uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi," aliongeza Gembe.

Kufuatia mafanikio hayo, Gembe aliuomba mradi wa SWIOfish kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi katika mwambao wa bahari wilayani humo ili rasilimali za uvuvi zilizopo ziendelee kuwanufaisha waliopo na vizazi vijavyo.

Aidha, aliwasihi wananchi wanaoishi katika mwambao wa bahari waliopata elimu hiyo ya utunzaji wa rasilimali za bahari na uoto wake waendelee kuienzi elimu hiyo kwa kuisambaza kwa wengine ili rasilimali hizo ziendelee kunufaisha jamii hizo na Taifa kwa ujumla.

Aliwakumbusha wananchi wa Wilaya hiyo kuwa mapambano dhidi ya uvuvi haramu sio nguvu ya soda ni mapambano endelevu na hawatakuwa na huruma na yeyote atakaye kwenda kinyume.

"Wananchi watambue kuwa tunafanya haya kwa nia njema, sisi tutaondoka lakini hii nchi itaendelea kuwepo, tufikirie Tanzania ya miaka 50 ijayo, tusiwe na mawazo ya kupata sasa tu, huo utakuwa ubinafsi," alifafanua Gembe.

Mkurugenzi huyo aliushukuru mradi wa SWIOfish kwa kuwapatia vifaa mbalimbali ambavyo vimeweza kuisaidia halmashauri hiyo kuvitumia katika kulinda rasilimali za bahari.

sha kilo chake.

tukio hilo.

wataarifishwa, mahakamani.



Mgombea wa urais kupitia Chama cha ADC, Queen Cuthbert Sendiga, akihutubia wananchi, wavuvi na wafanyabiashara wa soko la samaki Bagamoyo, mkoani Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgombea urais ADC aahidi wavuvi fursa

**Na Boniface Gideon,**
PWANI

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, amewaahidi wavuvi fursa ikiwa atachaguliwa.

Alitoa ahadi hiyo jana wilayani Bagamoyo mkoani Pwani alipokutana na kuzungumza na wavuvi ikiwa ni sehemu ya mikutano ya kampeni.

Akizungumza katika viwanja vya soko la samaki mjini Bagamoyo, Sendiga alisema Ilani ya chama hicho imeweka vipaumbele kwa ajili ya sekta ya uvuvi.

"Wavuvi ni kundi kubwa sana ambalo ukiwatengenezea maisha mazuri, mipango na taratibu tunatengeneza ajira nyingi sana za kutosha na zenye uhakika kwa sababu mvuvi akiumwa siku tatu ama siku nne hawezi kwenda kuvua tena," alisema.

Alisema chama chake kimejipanga kuboresha maisha ya mvuvi kwa kuwawezesha kuwapatia elimu ya uvuvi, zana na mikopo yenye riba nafuu.

"ADC chini ya uongozi wangu kwa miaka mitano tunaenda kuhakikisha mvuvi wa kitanzania anaenda kuwa mvuvi bora, mwenye kupatiwa elimu juu ya shughuli zake za uvuvi, mwenye kupatiwa vitendea kazi bora na kuondolewa tozo zisizoendana na uwezo wake wa kuvua, na cha mwisho anaenda kuongezewa thamani ya bidhaa zake zinazotoka baharini ili iweze kumkwamua kutoka alipo kimaisha," alisema Sendiga.

Aliongeza kuwa wavuvi kwa sasa wamekuwa wakipitia changamoto mbalimbali katika shughuli zao ikiwamo kuchomewa nyavu, na kwamba akiingia madarakani ataziondoa zote ili wavuvi wafanye shughuli zao bila vikwazo vyovyote.


IN THE RMS COURT / DISTRICT COURT OF MOSHI
AT MOSHI

MISC.CIVIL APPL/CASE/MATRIMONIAL CAUSE NO.17 OF 2019

COURAGE WORLDWIDE WC
(CWW)..............................PLAINTIFF/APPL.

VERSUS

SECAO BUILDERS CO- LTD & THE BOARD OF
REGISTERED..............................DEFENDANTTRUSTEES OF
MKOMBOZI CENTRE FOR STREET CHILDREN &
INDEPENDENT ANGENCIES &
COURT BROUKER LTDNOTICE OF MENTION/HEARING.

TO: THE BOARD OF REGISTERED STUSTED OF MKOMBOZI CENTRE FOR STREET CHILDREN

Take Notice that the above case has been fixed for hearing/mention/ruling judgement in the RMS court at Moshi on 15th the day of October 2020 at 9:00am Oclock in the forenoon.
You may appear in person or by advocate of agent duly authorized to do so and you are directed to produce on that day of document under which you intend to rely in support of your case
TAKE FURTHER NOTICE that, default of your appearance on that day before mension the court will proceed with the matter in your absence
A copy of the petition of appeal. Judgement and decree are attached hereto.
Given under my hand and seal of this Court this 2 day of October 2020

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE I/C
MOSHI

115929802



**KUPOTEA KWA PASPORT**



115929702

**DICKSON ELIAFIE LEMA**
Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye no, TAE 222513 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji October 2019 Dar Es Salaam. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
KL/MOS/RB/700049/2020


Scanned with CamScanner

UFUGAJI BORA MWANANCHI UK 5.

# Serikali kuanza ununuzi wa pamoja chanjo za mifugo

Mwandishi Wetu, Mwananchi

Kibaha. Katika jitihada za kumpunguzia mfugaji gharama hivyo kumwongezea tija, Serikali imesema inatarajia kuzindua mfumo wa pamoja wa kuagiza chanjo za mifugo kutoka nje.

Mpango huo umebainishwa jana na mkurugenzi wa huduma za mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga alipozungumza na waandishi waandishi wa habari kuhusu upatikanaji na uzalishaji wa chanjo hizo nchini.

"Tanzania ina mifugo mingi lakini changamoto kubwa inayowakabili wafugaji ni magonjwa ambayo hudhibitiwa zaidi kwa chanjo. Mwaka huu tutazindua mfumo wa ununuzi wa pamoja wa chanjo ili kupunguza gharama kwa mfugaji," alisema Profesa Nonga.

Mtaalamu huyo alisema soko la mazao ya mifugo ya Tanzania linazidi kuimarika sasa hivi hivyo ili kukidhi vigezo vya kimataifa ni lazima wanyama wapewe kinga ya kutosha kama inavyopendekezwa.

Kuhakikisha hilo linazingatiwa, alisema hakuna atakayeruhusiwa kuchinja, kusafirisha wala kuuza mnadani mfugo usiochanjwa. Kila atakayechanja mifugo yake, alisema atapewa kadi kuthibitisha hilo hivyo kuwa huru kuchinja au kuuza popote; ndani au nje ya Tanzania.

Adhabu ya kutozingatia hilo, kanuni za chanjo ya mifugo za mwaka 2020 zinasema mhusika anaweza kutozwa faini isiyopungua Sh500,000 na isiyozidi Sh10 milioni.

Katibu mkuu wa wizara hiyo, Profesa Elisante ole Gabriel alisema mkakati wa kuimarisha chanjo sio tu utaongeza tija kwa wafugaji bali utapunguza gharama za matibabu kwa binadamu kwani asilimia 60 ya magonjwa yake husababishwa na mifugo.

"Kwa mwaka Serikali inatumia Sh270 bilioni kununua dawa, iwapo magonjwa ya mifugo yatadhibitiwa gharama hizo zitashuka kwa asilimia 60 hivyo fedha zitakazookolewa kuelekezwa maeneo mengine," alisema Profesa Gabriel.

Jukumu la kuzalisha chanjo za mifugo lipo chini ya Taasisi ya Chanjo Kibaha iliyoanzishwa mwaka 2012 ambayo mpaka sasa inazalisha aina sita kati ya 13 za magonjwa yaliyowekewa kipaumbele kudhibitiwa.

Meneja wa taasisi hiyo, Dk Stella Bitanyi alisema wana uwezo wa kuzalisha dozi milioni 100 kwa mwaka lakini oda wanazopokea ni wastani wa milioni 60.

"Ufugaji bora una fursa ya kukuza ajira hasa kwa vijana. Wafugaji wawatumie wataalamu kutoa chanjo na kutibu mifugo yao," alisema Dk Stella.

**MKAKATI >**

## Taasisi ya Chanjo Kibaha

**Taasisi ilianzishwa ili kuzalisha chanjo zote muhimu kukidhi mahitaji nchini. Kila nchi yenye mifugo mingi huzalisha chanjo zake, Ethiopia na Botswana ni mifano.**

**Taasisi ya Chanjo Kibaha inazalisha chanjo ya mdondo au kideri ikiwafaa zaidi kuku wa kienyeji pamoja na chanjo ya kimeta, chambavu, kutupa mimba na mapafu ya ng'ombe.**

**Taasisi pia ipo kwenye maandalizi ya kuzindua chanjo ya homa ya mapafu ya mbuzi, sotoka y ambuzi na kondoo na kichaa cha mbwa. Baadaye, chanjo ya ndigana, miguu na mdomo, mapele ngozi na bonde la ufa zitazalishwa.**

Corona y

Mussa Juma, Mwananchi
mjuma@mwananchi.co.t

Arusha. Licha gamoto zilizosab na kuibuka kwa corona, chuo cha kilichopo jijini ha sema kimepata kufundishwa lu Kiswahili mtanda wanafunzi kutoka tofauti hasa ya Ula

Akizungumza mahafali ya 13, m

during the opening of Kabawa Festival Exhibition

challenges must be identi and addressed immediately.

# Schools benefit from milk plan to stir learning

**From HECKTON CHUWA in Hai**

THE Netherlands-based international development organisation, SVN, donated and facilitated the distribution of milk to 10 schools in Hai District in Kilimanjaro as part of this year's school milk feeding programme.

Speaking during the launch of the programme, SNV Deputy Project Manager, Pascal Tekwi said the school milk feeding programme was implemented in collaboration with the Hai District Council and the Kilimanjaro Dairy Cooperative Joint Enterprise through three dairy cooperative societies in the district.

"The distribution of milk to 10 schools - both primary and secondary schools - will benefit over 3,000 schoolchildren by improving their health and learning capacity," he said.

He said apart from the school milk programme, SNV had also been involved in facilitating the development of dairy cooperative societies through different programmes, including those based on entrepreneurship education.

"We have so far disbursed 4,783,700/- to Ng'uni Dairy Cooperative, 4,350,000/- to Marukeni Dairy Co-operative and 6,732,000/- to Kalali Dairy Co-operative to facilitate milk processing education through Small Industries Development Organisation (SIDO)," he noted.



PE
Co
se